**AZIMIO LA BUNGE NA. ..........................................LA MWAKA 2023**

**AZIMIO LA BUNGE LA MAPENDEKEZO YA TANZANIA KURIDHIA MKATABA WA WAKALA WA KIMATAIFA WA NISHATI JADIDIFU (STATUTE OF THE INTERNATIONAL RENEWABLE ENERGY AGENCY- IRENA)**

**KWA KUWA,** Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni miongoni mwa Nchi Wanachama wa Umoja wa Mataifa ambapo Tanganyika ilikuwa mwanachama wa Umoja wa Mataifa tangu tarehe 14 Desemba 1961 na Zanzibar ilikuwa mwanachama tangu tarehe 16 Desemba 1963. Baada ya kuridhia Ibara za Muungano kati ya Tanganyika na Zanzibar tarehe 26 Aprili 1964, Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar iliendelea kama mwanachama mmoja, ikibadilisha jina lake kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 1 Novemba 1964.

**NA KWA KUWA,** Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni miongoni mwa Nchi Mwanachama wa taasisi za ushirikiano wa kiuchumi wa kikanda wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (Southern African Development Community- (SADC) kupitia Azimio la Bunge lililopitishwa tarehe 27 Agosti,1993 na Hati iliyowasilishwa Sekretarieti ya Jumuiya hiyo mnamo tarehe 5 Septemba, 1993.

**NA KWA KUWA,** kwa kutambua malengo yaliyomo katika Mkataba wa Wakala wa Kimataifa wa Nishati Jadidifu (IRENA) iliyoanzishwa tarehe 26 Januari 2009 ikiwa na malengo ya kuendeleza na kuhamasisha matumizi endelevu ya aina zote za nishati jadidifu, kwa kuzingatia vipaumbele vya taifa na manufaa yatokanayo na kukuza nishati hiyo, pamoja na mchango wake katika kuhifadhi mazingira hususani kukabiliana na uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi; kukuza uchumi na kupunguza umaskini pamoja na usalama katika upatikanaji wa nishati.

**NA KWA KUWA**, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ina raslimimali za nishati jadidifu katika maeneo mbalimbali ya nchi na sera ya Taifa ya mwaka 2015 inayotambua rasimilimali kubwa ya nishati jadidifu iliyopo nchini ikiwemo upepo, jua, tungamotaka, maporomoko madogo ya maji, jotoardhi na mawimbi ya bahari, inapaswa kuridhia mkataba huu ili iweze kunufaika na manufaa yatokanayo na rasilimali za nishati hizo jadidifu.

**NA KWA KUWA** madhumuni na misingi ya mkataba wa Wakala wa Kimataifa wa Nishati Jadidifu (IRENA) ni pamoja na –

(a) kuhamasisha, kupanua na kuongeza matumizi endelevu ya vyanzo vyote vya Nishati Jadidifu kwa kuzingatia vipaumbele vya taifa.;
(b) kuhifadhi mazingira;

(c) kukabiliana na uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi;
(d) kukuza uchumi na kupunguza umaskini; na
(e) kuhakikisha usalama katika upatikananji wa nishati

**NA KWA KUWA,** kuridhiwa kwa Mkataba huu kutakuwa na manufaa yafuatayo kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania-

(a) kuimarika kwa kasi ya uendelezaji wa rasilimali za Nishati jadidifu zilizopo nchini;
(b) kuimarika kwa utaalamu ,teknolojia, utafiti na uelewa kuhusu Nishati jadidifu kwa watoa maamuzi na wadau mbalimblai wa anishati
(c) Nchi kupata taarifa na takwimu sahihi kuhusu masuala ya Nishati jadidifu na pia fursa za kuwekeza katika nchi zingine;
(d) Kuimarika kwa uwekezaji, mitaji na upatikanaji wa ushauri wa kiufundi katika uendelezaji wa Nishati jadidifu nchini;
(e) Kuimarika kwa upatikanaji wa nishati ya gharama nafuu na rafiki wa mazingira ambayo ni kichocheo cha ukuaji wa uchumi na kupunguza umasikini;
(f) Kupungua kwa uharibifu wa mazingira unaotokana na uzalishaji na matumizi ya nishati isiyo rafiki kwa mazingira na pia kukabiliana na mabadiliko ya tabia ya nchi; na
(g) Kuimarisha kasi ya utekelezaji wa matumizi ya vyanzo vya nishati visivyoathiri mazingira na kusababisha mabadiliko ya tabia ya nchi kuendana na mwelekeo wa dunia wa sasa.

**HIVYO BASI,** kwa kuzingatia manufaa ambayo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itayapata kutokana na Mkataba huu, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wake wa 12 na kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, linaazimia kuridhia Mkataba kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Taasisi ya Wakala wa Kimataifa wa Nishati Jadidifu Kuhusu ushirikiano wa kiuchumi na kwa ajili ya uendelezaji na Nishati Jadidifu.